# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KUMI

**12 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KUMI – TAREHE 12 FEBRUARI, 2024

**I. DUA:**

**II. TAARIFA YA SPIKA:**

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## IV. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**156. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Utiri iliyopo Jimbo la Mbinga Mjini.

**157. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanzisha Tarafa mpya Mtwara kwa kuwa Halmashauri ya Mtwara ilipogawanywa ilijitokeza changamoto ya mipaka ya Tarafa.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**158. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini ujenzi wa Jengo la TAKUKURU Wilaya ya Mbulu utaanza.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**159. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wanaume wanaozitelekeza familia zao baada ya Mke kujifungua Watoto mapacha kuanzia watatu.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**160. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kuna Mkakati gani kuhakikisha Kiwanda cha kuchakata mazao ya Karanga, Ufuta na Alizeti kinajengwa Kata ya Likokona Nanyumbu.

**161. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, nini mpango wa Serikali kuanzisha kiwanda cha kutengeneza Pikipiki nchini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**162. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wakulima wa Tumbaku Urambo ambao hawajalipwa fedha zao kwa muda mrefu.

**WIZARA YA AFYA:**

**163. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuruhusu Sayana Press kama njia ya uzazi wa mpango badala ya kutumia P2 bila utaratibu.

**WIZARA YA NISHATI:**

**164. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini ahadi ya kupeleka umeme wa REA kwenye Wilaya za Mkoa wa Mbeya itakamilika.

**WIZARA YA FEDHA:**

**165. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali imeshalipa Wazabuni wangapi wanaodai katika Taasisi mbalimbali nchini na ni kiasi gani kimeshalipwa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**166. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini minara ya mawasiliano itajengwa katika Kijiji cha Msasa Kata ya Busanda na Kijiji cha Nyakagomba Kata ya Nyakagomba.

**WIZARA YA MAJI:**

**167. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa kusambaza maji katika Tarafa ya Turiani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**168. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga upya Uwanja wa Mpira katika Chuo cha Ualimu Patandi kufuatia kujengwa Mabweni ya Shule kwenye uwanja uliokuwepo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**169. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Fidia kwa waathirika wa Wanyamapori ili kulipa fidia ya gharama halisi tofauti na sasa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**170. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga Majosho kwenye Vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki ili kulinda afya za Mifugo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**171. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kukomesha migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji Wilayani Kilwa.

## V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **12 FEBRUARI, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA